

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA KWIMBA**



**TANZIA**



Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba, Bibi Pendo A. Malabeja anasikitika kutangaza kifo cha **Mhe. Diwani Julius Samamba Nyeye** wa Chama cha Wananchi - CUF kata ya Lyoma Jimbo la Sumve Wilaya ya Kwimba, kilichotokea alfajiri siku ya Jumanne tarehe 16/01/2018 katika Hospitali ya Rufaa Bugando Mkoa wa Mwanza alipokuwa akipata matibabu.

Mkurugenzi Mtendaji anawapa pole Familia, Baraza la Waheshimiwa Madiwani, Viongozi mbalimbali, Watumishi, Ndugu, Jamaa na Marafiki wa Marehemu. Mungu awape moyo wa Uvumivu katika kipindi hiki kigumu cha majonzi.

Mwili wa Marehemu unatarajiwa kuzikwa tarehe 19 Januari, 2018 siku ya Ijumaa saa 8:00 mchana katika kijiji cha Kimiza Kata ya Lyoma Wilayani Kwimba.

Bwana ametoa na Bwana ametwaa, Jina la Bwana lihimidiwe. Amina

**Imetolewa na:**

Kitengo cha TEHAMA na Uhusiano,  
Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba,  
Tarehe 17 Januari, 2018.